



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA
KUSITISHA MKATABA NA VITUO VYA MATIBABU KUTOKANA NA VITENDO VYA UDANGANYIFU

Dodoma, Alhamisi, Januari 19, 2023:

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unapenda kuwatangazia Wanachama wake na Umma kuwa imesitisha mkataba wa kutoa huduma za matibabu kwa wanachama wake kwa vituo tisa kutokana na kuwasilisha madai ya malipo ya huduma yaliyobainika kuwa na udanganyifu.

Mojawapo ya wajibu wa Mtoa huduma za matibabu aliyeingia mkataba na NHIF kuhudumia wanachama, ni kuwasilisha madai sahihi kwa NHIF kwa ajili ya malipo. Mfuko una wajibu wa kuchukua hatua stahiki kwa vituo vinavyobainika kufanya udanganyifu ikiwa ni pamoja na kusitisha mkataba na kuwasilishwa kwenye mamlaka za kisheria kwa hatua zaidi.


Vituo vifuatavyo vimesitishiwa mkataba:-

Na.	Jina la Kituo	Mkoa
1	Ruvuma Polyclinic	Ruvuma
2	Ruvuma Pharmacy	Ruvuma
3	St. Benjamin Dispensary	Ruvuma
4	Good Samaritan Charitable H/C	Geita
5	Muhali Diabetic and Endocrinology Clinic	Dar es salaam
6	P. Consultant Polyclinic (Kigamboni)	Dar es salaam
7	Health Scope Dispensary	Dar es salaam
8	Bethlehem Dental Clinic	Tanga
9	Face Specialized Dental Clinic (Temeke)	Dar es salaam

Kwa taarifa hii, Mfuko unawataarifu wanachama wake kutumia vituo vingine vyenye mkataba na NHIF vilivyo kwenye maeneo yao kupata huduma za matibabu kwa kutumia kadi zao za NHIF.

Aidha, Mfuko unaendelea kuwatahadharisha Watoa huduma wenye mikataba na NHIF kutojihusisha na vitendo vya udanganyifu, na Mfuko utaendelea kuchukua hatua kwa vituo vinavyobainika kufanya udanganyifu.

Imetolewa na,


Anjela A. Mziray
MENEJA UHUSIANO